Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Dokeza la wenye akili

'Allāmā Tabātabāi katika kitabu chake 'Al-Mizān' anasema kitu muhimu sana cha kutafakari: "Wakati Zulaykha alipofunga kabisa milango ya chumba chake (*ghallaqat al-abwāb*), na kutegemea juu ya uwezo wa dhahiri ambao alikuwa nao, alisema: *'hayta lak'* (njoo [kwangu!]), Yusufu (a.s.) alikuwa amezama katika mapenzi ya Allah (s.w.t.) na akasahau kila njia ya wazi ya hifadhi, pamoja na yeye mwenyewe; kwa hiyo wakati akiomba hifadhi kwa Allah (s.w.t.) kamwe hasemi *'Inni a'ādhu'* (hakika mimi naomba hifadhi) lakini alisema 'ma 'ādhallāh!' [Tanbihu: ingawa zote *a'ādhubillāhi na ma'ādhallāh* huonyesha kwamba Yusufu anaomba hifadhi kwa Allah, lakini neno hili la mwisho (yaani: ma'ādhallāh) muombaji husahau njia zote za wazi za hifadhi, pamoja na yeye mwenyewe]

'Allāma Tabātabāi anasema:

...فَلَمْ يَقُلْ: إِنِّيْ أَعُوْذُ مِنْكَ بِاللّهِ أَوْمَا يُؤَدِّيْ مَعْنَاهُ، وَ إِنَّمَا قَالَ:مَعَاذَ اللّه...

"...yeye [Mtume Yusufu (a.s.)] hakusema: Hakika mimi naomba hifadhi kwa Allah kutokana na wewe..." au maelezo yanayofanana na hayo; bali amesema tu: 'ma'aadhallah' (hivyo bila kutaja 'mimi' au 'wewe' au njia yoyote nyingine)..."[1]

Kisha 'Allama akaendelea kusema:

و كمْ مِنَ الْفَرْق بَيْنَ قَوْلِهِ هَذَاَ وَ بَيْنَ قَوْلِ مَرْيَم للرُوح لَما تَمَثَّلَ لَهَا.....

بَشَرا سَويا : إِنِّي أَعُوذُ بِالرَّحْمَٰنِ مِنْكَ....

"...Na ukubwa ulioje wa tofauti kati ya kauli yake hii na kauli ya Mariamu kwa Roho Mtakatifu wakati alipojitokeza kwake katika umbo la mwanadamu: ***'Hakika najilinda kwa Mwingi wa rehema...' "*** [***19: 18***]

1. Allama Tabtabai, Al-Mizan, j. 11 uk. 120-123.

Source URL: https://www.al-islam.org/fr/node/39635#comment-0